

KOROSHO COOPERATIVE JOINT ENTERPRISE LIMITED



Head Office:

TIN No. 167-403-670 Maduka Makubwa, TANECU HOUSE
REG No. AFF-MTR-MC-2023-104 P. O. Box 310, Mtwara
Mobile No. +255738481316 Email: info@koroshocje.coop
Website: www.koroshocje.coop

TANGAZO LA ZABUNI

1. Mradi wa Pamoja wa Vyama vya Ushirika wa Korosho (KCJE) unatangaza zabuni ya Pembejeo kwa ajili ya msimu wa kilimo kwa mwaka **2027/2028 zabuni na (KCJE/2027/2028/G/02)**.
2. Kwa idhini ya Bodi ya Mradi wa Pamoja KCJE LTD. Mwenyekiti wa Bodi anatangaza zabuni shindani ya Kitaifa kwa ajili ya ununuzi wa pembejeo za kilimo.
3. Mchakato wa zabuni hii utafanyika kwa mujibu wa Mwongozo wa Manunuzi wa Vyama vya Ushirika Tanzania Bara.
4. Nyaraka zitanunuliwa na wazabuni wenye nia baada ya kulipa ada isiyorejeshwa ya TZS 5,000,000 (Milioni tano) kupitia akaunti ya **CRDB Namba 0150771321300 (KOROSHO COOPERATIVE JOINT ENTERPRISE LIMITED)**.
5. Waombaji wawasilishe zabuni zao katika Ofisi ya Mradi wa Pamoja, nakala halisi moja (1) na nakala kivuli mbili (2) zikiwa zimefungwa vizuri kwenye bahasha na kutiwa **lakiri** na kuainisha namba ya zabuni juu ya bahasha ya maombi yake.
6. Muda wa kutuma maombi ya zabuni ni siku kumi na nne (14) baada ya tangazo kutolewa, na ufunguzi wa zabuni utafanyika siku ya Jumanne tarehe 20.10.2026 saa 5.00 asubuhi mbele ya wazabuni na wawakilishi watakaohudhuria ufunguzi huo, ambao utafanyika katika ukumbi wa **Eden Beach House Mtwara**. Zabuni zitakazochelewa hazitafanyiwa kazi.
7. Baada ya kulipia kabrasha la zabuni tuma risiti yako kupitia barua pepe za ofisi ambazo zinapatikana juu ya tangazo hili pamoja na mawasiliano ya upatikanaji wa kabrasha la zabuni.

TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA

O. Odani

.....
ODAS MPUNGA

MWENYEKITI WA BODI

KOROSHO COOPERATIVE JOINT ENTERPRISE LIMITED.

